SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA BODI YA MAPATO ZANZIBAR, NAM. 7 YA 1996 NA KUANZISHA MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR KAMA CHOMBO KIKUU CHA KUFANYA TATHMINI NA KUKUSANYA MAPATO YALIYOAINISHWA ILI KUSIMAMIA NA KUTEKELEZA SHERIA ZINAZOSIMAMIA MAPATO HAYO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


VIFUNGU MAELEZO

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA KWA MAMLAKA

3. Kuanzishwa kwa Mamlaka.
4. Muhuri na Nembo ya Mamlaka.
5. Kazi za Mamlaka.
6. Uwezo wa Mamlaka.
7. Uwezo wa Waziri kuipangia Mamlaka.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAMLAKA

8. Kuanzishwa kwa Bodi.
9. Sifa za Mwenyekiti.
10. Makamu Mwenyekiti.

11. Katibu wa Bodi.

12. Kazi za Bodi.

13. Uwezo wa Bodi.

14. Kamati za Bodi.

15. Posho la Wajumbe.

16. Mwenendo wa Bodi.

17. Uteuzi wa Kamishna Mkuu.

18. Sifa za Kamishna Mkuu.

19. Kukasimu uwezo na kazi.

20. Idara, divisheni na Vitengo vya Mamlaka.

21. Wafanyakazi wa Mamlaka.

22. Maslahi.

**SEHEMU YA NNE**
**MASHARTI YA FEDHA**

23. Mapato kuingizwa katika akaunti ya Serikali.

24. Fedha za Mamlaka.

25. Makadirio ya bajeti.

26. Hesabu na ukaguzi.

27. Ukaguzi wa ndani na ripoti za ukaguzi za muda.

28. Ripoti za Kamishna Mkuu.

29. Kufuta kodi isiyoweza kugombolewa.

30. Mamlaka kusamehewa kodi.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI MENGINEYO

31. Kinga ya kutowajibika binafsi.

32. Kuomba msaada.

33. Utambuzi wa walipakodi.

34. Usiri.

35. Ukabidhiwaji wa mali na waajiriwa.

36. Utekelezaji wa amri dhidi ya Mamlaka.

37. Uwezo wa kurekebisha majadweli.

38. Kufuta na kubakiza.

39. Kanuni.

40. Marekebisho yenye athari.

## MAJADWELI

**SHERIA NAM. 11 YA 2022**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

29 Disemba, 2022

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA BODI YA MAPATO ZANZIBAR, NAM. 7 YA 1996 NA KUANZISHA MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR KAMA CHOMBO KIKUU CHA KUFANYA TATHMINI NA KUKUSANYA MAPATO YALIYOAINISHWA ILI KUSIMAMIA NA KUTEKELEZA SHERIA ZINAZOSIMAMIA MAPATO HAYO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar, 2022 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais na kutangazwa katika Gazeti.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yanahitaji vyenginevyo:

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Mapato Zanzibar iliyoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka iliyoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Kamishna Mkuu" maana yake ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka aliyeteuliwa chini ya masharti ya Sheria hii na itajumuisha mtu mwengine yeyote ambaye amekasimiwa kazi na uwezo na Kamishna Mkuu;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na fedha;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Mapato" maana yake ni kodi, ushuru, ada, faini, adhabu au tozo nyengine zilizotozwa na au zinazolipwa chini ya sheria zinazohusiana na mapato ya Zanzibar kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii au kama itavyopangiwa Mamlaka kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"Mlipakodi" ina maana kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Usimamizi na Taratibu za Kodi.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA MAMLAKA

Kuanzishwa kwa Mamlaka.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Mamlaka itakayojulikana kama Mamlaka ya Mapato Zanzibar na ufupisho wake utakuwa ni "ZRA".

(2) Mamlaka itakuwa ni chombo kinachojitegemea chenye urithi wa kuendelea, chenye muhuri na kwa jina lake kitakuwa na uwezo wa:

(a) kushitaki na kushitakiwa;

(b) kuingia katika mkataba au muamala wowote;

(c) kupata, kununua, kumiliki na kuondosha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(d) kukopa, kukopesha au kupokea msaada wa kiwango chochote cha fedha kutoka taasisi yoyote ya fedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(e) kutekeleza au kufanya kitendo au jambo lolote ambalo Mamlaka kwa asili yake inaweza, kulitekeleza kwa mujibu wa Sheria.

Muhuri na Nembo ya Mamlaka.

**4.**-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Mamlaka katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Mamlaka katika waraka wowote yatathibitishwa na saini ya Kamishna Mkuu au Kamishna yeyote wa Mamlaka aliyeidhinishwa na Kamishna Mkuu.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Mamlaka utawekwa muhuri wa Mamlaka na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Kazi za Mamlaka.

**5.** Kazi za Mamlaka ni:

(a) kusimamia na kuhakikisha usawa, uwazi, ubora na ufanisi wa usimamizi na utekelezaji wa:

(i) sheria au masharti yaliyoainishwa katika sheria yanayohusiana na ukusanyaji wa mapato Zanzibar kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii au kama itakavyopangiwa Mamlaka kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(ii) sheria nyengine yoyote inayohusiana na ukusanyaji wa mapato ambayo itapangiwa Mamlaka na wizara, idara au mamlaka yoyote inayosimamia sheria hiyo;

(b) kutathmini, kukusanya na kuwajibika kwa mapato yote yaliyoainishwa na sheria katika aya ya (a) ya kifungu hiki;

(c) kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari kwa kuwahusisha walipakodi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kiwango cha juu kwa kadri itakavyowezekana;

(d) kuweka na kuhifadhi takwimu za ukusanyaji wa mapato;

(e) kuchukua hatua kama itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya kuimarisha kiwango cha huduma kinachotolewa kwa walipakodi na Mamlaka, kwa lengo la kuimarisha ufanisi;

(f) kuainisha hatua zitakazochukuliwa za kudhibiti udanganyifu na aina nyengine za ukwepaji kodi na fedha;

(g) kufanya tafiti zinazohusiana na masuala ya kodi na ukusanyaji wa mapato ili kumshauri Waziri na taasisi nyengine husika za Serikali;

(h) kukusanya na kuchakata takwimu zinazohitajika kupanga malengo ya mapato na athari ya matokeo inayotokana na mapendekezo ya marekebisho katika sheria za mapato;

(i) kumshauri Waziri na taasisi nyengine husika za Serikali katika mambo yanayohusiana na sera za kifedha, usimamizi wa kodi na mapato ya Serikali;

(j) kuweka malengo, kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu na mafunzo kwa maafisa wake na waajiriwa wengine;

(k) kuhakikisha uwajibikaji kwa watendaji wake katika sheria za mapato kwa kiwango cha hali ya juu; na

(l) kufanya kazi nyengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Waziri.

Uwezo wa Mamlaka.

**6.**-(1) Mamlaka, katika kutekeleza kazi zake itakuwa na uwezo wa:

(a) kuchukua hatua stahiki kudhibiti ukwepaji kodi, uepukaji wa kodi na upotevu wa mapato ya Serikali;

(b) kuanzisha na kuweka mifumo kwa ajili ya kuwatambua walipakodi na ukusanyaji wa mapato kwa madhumuni ya usimamizi wa sheria za mapato Zanzibar na itakuwa na uwezo wa kuchukua hatua zitakazohitajika kwa mujibu wa masharti ya sheria zilizoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii;

(c) kuchambua sheria za mapato na kuainisha marekebisho au mabadiliko yanayoweza kufanywa katika sheria yoyote kwa madhumuni ya kuimarisha usimamizi na uwajibikaji wa sheria za mapato;

(d) kutathmini, kukusanya na kuwasilisha mapato yote yaliyotozwa chini ya sheria zisizo za kodi zitakazopangiwa Mamlaka;

(e) kutumia mali zote za Mamlaka zinazohamishika na zisizohamishika kwa namna itakavyoonekana inafaa ikiwa ni pamoja na kutafuta mikopo kwa kuweka rehani mali hiyo;

(f) kufanya shughuli nyengine yoyote katika kuimarisha uelewa wa kodi miongoni mwa walipakodi; na

(g) kufanya jambo jengine lolote lililopo chini ya uwezo wake.

(2) Katika kusimamia utekelezaji wa masharti ya kifungu kidogo cha (1)(d) cha kifungu hiki, masharti husika ya Sheria ya Usimamizi na Taratibu za Kodi juu ya tathmini, ukusanyaji, njia za kugomboa kodi, pingamizi za kodi na makosa, pamoja na masharti ya rufaa yaliyoainishwa katika Sheria ya Rufaa za Kodi yatatumika sawa.

(3) Endapo kutatokea mgongano baina ya masharti ya Sheria hii na masharti ya sheria zisizo za kodi zilizoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1)(d) cha kifungu hiki, masharti ya Sheria hii yatatumika.

Uwezo wa Waziri kuipangia Mamlaka.

**7.** Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Waziri anayehusika na sheria zisizokuwa za kodi, kuipangia Mamlaka usimamizi wa mapato yoyote yanayotozwa chini ya sheria zisizokuwa za kodi.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAMLAKA

Kuanzishwa kwa Bodi.

**8.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais;

(b) Kamishna Mkuu;

(c) Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar au mwakilishi wake;

(d) Katibu Mkuu anayehusiana na masuala ya fedha au mwakilishi wake;

(e) mjumbe mmoja kutoka katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(f) wajumbe wengine wawili wenye taaluma na uzoefu katika masuala ya uhasibu, usimamizi wa biashara, fedha, biashara, uchumi, kodi, teknolojia ya habari na mawasiliano au sheria, ambao hawana maslahi katika Mamlaka.

(2) Wajumbe chini ya aya ya (e) na (f) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na Waziri husika kwa kuzingatia uzoefu, ujuzi, utaalamu na mgawanyo wa jinsia.

(3) Isipokuwa mjumbe chini ya aya ya (e) ya kifungu hiki na wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao anaweza kuhudhuria vikao vya Bodi yeye mwenyewe au mwakilishi aliyeteuliwa, isipokuwa kwamba mwakilishi aliyeteuliwa awe na cheo cha Afisa Mwandamizi au zaidi.

Sifa za Mwenyekiti.

**9.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya kodi, uhasibu, usimamizi wa biashara, fedha, biashara, uchumi au sheria kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(c) ana uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba na kiwango cha juu cha uweledi wa kusimamia kwa ufanisi masuala ya taasisi za umma au binafsi; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu.

Makamu Mwenyekiti.

**10.** Wajumbe wa Bodi watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Katibu wa Bodi.

**11.**-(1) Bodi itamteua mtumishi wa umma kutoka miongoni mwa wafanyakazi wa Mamlaka kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuwa Katibu wa Bodi ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria; au mwenye sifa ya kuwa katibu wa shirika kutoka katika taasisi inayotambulika na Serikali; na

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika utumishi wa umma.

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi, na:

(a) ataandaa agenda za vikao vya Bodi kwa kushauriana na Mwenyekiti.

(b) atachukuwa kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(c) atatunza taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(d) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe;

(e) atatoa ushauri sahihi kwa Bodi pale unapohitajika; na

(f) atafanya kazi nyengine zozote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Kazi za Bodi.

**12.** Kazi za Bodi zitakuwa ni:

(a) kuandaa, kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa Sera za Mamlaka;

(b) kuidhinisha bajeti, kanuni za fedha na mpango kazi wa Mamlaka;

(c) kusimamia masuala yote yanayohusiana na usimamizi wa Mamlaka na ukusanyaji wa mapato chini ya Sheria hii;

(d) kutoa miongozo ya kimkakati kwa Mamlaka;

(e) kusimamia maadili, uweledi na uadilifu wa wafanyakazi wa Mamlaka;

(f) kuhakikisha kwamba Mamlaka inafuata mpango mkakati, mpango wa kupunguza athari na hatua zinazolenga kukuza utendaji;

(g) kuchukua hatua dhidi ya watumishi wa Mamlaka wenye makosa ili waendane na sheria zilizopo, kanuni, kanuni za maadili na viwango vya utendaji vinavyohitajika;

(h) kupendekeza marekebisho katika sheria na kanuni zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato Zanzibar; na

(i) kumshauri Waziri na taasisi nyengine za Serikali zinazohusika katika masuala yanayohusiana na sera za fedha na usimamizi wa kodi.

Uwezo wa Bodi.

**13.**-(1) Bodi, katika kutekeleza kazi zake, itakuwa na uwezo wa:

(a) kumuelekeza Kamishna Mkuu kuipatia taarifa yoyote, ripoti au nyaraka nyengine ambazo Bodi itaona ni muhimu katika utekelezaji wa kazi zake;

(b) kutoa maelekezo halali kwa Kamishna Mkuu kuhusiana na uendeshaji na utendaji wa Mamlaka;

(c) kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, kuidhinisha muundo wa taasisi na taratibu za kazi kama itakavyoonekana inafaa kwa utekelezaji bora wa kazi na majukumu ya Mamlaka;

(d) kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, kuamua vigezo na masharti ya utumishi, kanuni za wafanyakazi, mishahara na posho ikijumuisha na maslahi mengine yoyote kwa Kamishna Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi, Meneja, wakuu wa vitengo na waajiriwa wa Mamlaka;

(e) kuidhinisha mipango kazi na malengo kwa idara au vitengo vyote na kusimamia maendeleo yao katika kuyafikia kwa utaratibu endelevu;

(f) kubuni na kuandaa mfumo wa ulinzi kupitia mifumo ya ukaguzi wa ndani na kuhakiki usahihi wa mwenendo wa idara za mapato katika kesi mbali mbali zilizopo na kwa mujibu wa sheria na miongozo ya Waziri;

(g) kuchukua hatua stahiki za kuwarekebisha wafanyakazi wa Mamlaka kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Kanuni za Wafanyakazi na Kanuni za Maadili;

(h) kusimamia maadili ya kazi, nidhamu na viwango vya kitaalamu kwa waajiriwa wa Mamlaka; na

(i) kuidhinisha bajeti ya matumizi ya mwaka ya Mamlaka.

(2) Isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo katika Sheria hii au sheria nyengine yoyote inayotumika kwa wakati huu, Bodi haitokuwa na uwezo wa:

(a) kuingilia katika kuamua deni la kodi kwa mlipakodi husika;

(b) kupata taarifa yoyote kuhusu deni au vyenginevyo la mtu yoyote katika kodi.

(3) Bodi inaweza kutoa maelekezo ya jumla kwa kuiongoza Mamlaka na inaweza kugundua makosa kupitia mfumo wa ukaguzi wa ndani na kutoa miongozo sahihi ya kurekebisha ambayo itatakiwa kufuatwa na wahusika wote.

Kamati za Bodi.

**14.**-(1) Bodi inaweza kuanzisha kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi mahsusi kama itakavyoona inafaa.

(2) Wajumbe wa Kamati watakuwa miongoni mwa wajumbe wa Bodi tu isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo na sheria nyengine inayotumika.

Posho la wajumbe.

**15.** Mwenyekiti na Wajumbe wengine watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na sheria nyengine zinazohusika.

Mwenendo wa Bodi.

**16.** Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi yatakuwa kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii.

Uteuzi wa Kamishna Mkuu.

**17.**-(1) Kutakuwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Kamishna Mkuu atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu na atawajibika kwa usimamizi wa utekelezaji wa kazi za kila siku za Mamlaka.

Sifa za Kamishna Mkuu.

**18.** Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Kamishna Mkuu ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya kodi, uhasibu, usimamizi wa biashara, fedha, biashara, uchumi au sheria kutoka katika taasisi inayotambulika na Serikali;

(b) ana uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba; na

(c) ana uadilifu wa hali ya juu.

Kukasimu uwezo na kazi.

**19.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza, kwa kuzingatia sheria au maelekezo yoyote ya Waziri au Bodi, kukasimu uwezo na kazi zake kuhusiana na usimamizi wa sheria za mapato kwa Kamishna yeyote, Mkurugenzi, Meneja au Afisa wa Mamlaka.

(2) Kwa kuzingatia maelekezo yoyote ya Kamishna Mkuu, kinyume chake, uwezo na majukumu yoyote ya Kamishna Mkuu chini ya Sheria hii yanaweza kutekelezwa na afisa yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi kwa niaba ya Kamishna Mkuu.

(3) Bila ya kujali chochote kilichomo katika sheria nyengine yoyote:

(a) afisa yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi kwa niaba ya Kamishna Mkuu anaweza kuhudhuria katika mahkama yoyote kwa niaba ya Kamishna Mkuu katika shauri lolote ambalo Kamishna Mkuu ni sehemu; na

(b) kwa kuzingatia maelekezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka, afisa yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi kwa niaba ya Kamishna Mkuu anaweza kuendesha mashtaka yoyote kwa kosa lolote chini ya sheria yaliyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii na kwa madhumuni hayo atakuwa na uwezo wote wa mwendesha mashtaka aliyeteuliwa chini ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai.

(4) Endapo chombo cha mahkama au chombo chengine chochote cha uchunguzi kitamuita Kamishna Mkuu kuhudhuria au kueleza katika jambo lolote linalohusiana na usimamizi wa kodi, Kamishna Mkuu au afisa yeyote wa cheo cha Afisa Mkuu au zaidi anaweza kuhudhuria au kueleza kama itakavyokuwa.

Idara, divisheni, na vitengo vya Mamlaka.

**20.**-(1) Mamlaka inaweza kuanzisha idara, divisheni na vitengo itakapoona inafaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Makamishna na Wakurugenzi wa idara watateuliwa na Bodi kwa kuzingatia utaratibu wa ushindani utakaowekwa na Bodi.

(3) Mameneja na Wakuu wa Vitengo watateuliwa na Kamishna Mkuu kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(4) Makamishna, Wakurugenzi, Mameneja na Wakuu wa Vitengo watawajibika kwa Kamishna Mkuu.

Wafanyakazi wa Mamlaka.

**21.** Kutakuwa na wafanyakazi wa Mamlaka watakaoajiriwa chini ya vigezo na masharti kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Maslahi.

**22.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Mamlaka itakuwa na vigezo na masharti yao ya utumishi, mishahara na posho ikijumuisha maslahi yoyote kwa Kamshina Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi, Mameneja na Wakuu wa Vitengo, Maafisa na wafanyakazi wengine wa Mamlaka.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA FEDHA

Mapato kuingizwa katika akaunti ya Serikali.

**23.**-(1) Mapato yote yanayokusanywa au kulipwa kwa Mamlaka chini ya sheria yoyote ya mapato yatawekwa katika akaunti ya Serikali kwa mujibu wa taratibu za Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(2) Kamishna Mkuu atawasilisha kwa Bodi ripoti ya kila mwezi kuhusiana na mapato yaliyokusanywa.

Fedha za Mamlaka.

**24.**-(1) Fedha za Mamlaka zitajumuisha:

(a) kiwango cha fedha kitakachoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) kiasi kinachoweza kupatikana kwa kubakiza asilimia fulani ya mapato yanayokusanywa na Mamlaka kama itakavyoamuliwa mara kwa mara na Waziri; na

(c) kiwango cha fedha kitakachopokelewa au watakachopewa Mamlaka kwa njia ya ruzuku, mikopo, ada, riba au kiwango chengine cha fedha kwa madhumini ya kutekeleza kazi zake kwa kuzingatia idhini ya Waziri.

(2) Mamlaka inaweza kutoza na kukusanya ada kuhusiana na machapisho ya programu za mafunzo, semina, ushauri na huduma nyengine zinazotolewa na Mamlaka.

(3) Matumizi yote ya Mamlaka yatatoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina Zanzibar na Serikali itaweka fungu la kutosheleleza katika bajeti yake ya mwaka ili kuhakikisha fedha zinapatikana kwa Mamlaka.

Makadirio ya bajeti.

**25.**-(1) Kamishna Mkuu, si zaidi ya miezi mitatu kabla ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, ataandaa na kuwasilisha kwa Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha unaofuata, ambayo baada ya kuidhinishwa, itapelekwa kwa Waziri kwa ajili ya kujumuishwa katika bajeti ya mwaka ya Serikali.

(2) Kamishna Mkuu anaweza wakati wowote kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha, kuandaa na kuwasilisha kwa Bodi kwa ajili ya idhini ya makadirio yoyote ya ziada kwa makadirio ya mwaka wa fedha uliopo.

(3) Matumizi hayatofanywa nje ya fedha za Mamlaka isipokuwa matumizi hayo ni sehemu ya matumizi yaliyoidhinishwa na Bodi chini ya makadirio kwa mwaka wa fedha ambapo matumizi yatafanyika au katika makadirio ya ziada kwa mwaka huo.

Hesabu na ukaguzi.

**26.**-(1) Mamlaka itaweka hesabu na kumbukumbu za miamala yake na itahakikisha kwamba fedha zote zilizopokelewa na zilizolipwa kwa niaba yake zinawekwa katika hesabu, zimeidhinishwa na udhibiti wa kutosha unawekwa juu ya mali na madeni yake.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi itaweka taratibu zinazojitosheleza za kifedha na mifumo ya ukaguzi wa ndani na Kamishna Mkuu atakuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba taratibu hizi zinafuatwa ipasavyo na wote wanaohusika.

(3) Hesabu za mwaka za Mamlaka zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ukaguzi wa ndani na ripoti za ukaguzi za muda.

**27.** Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani, pamoja na kazi nyengine atakazopangiwa na Bodi au Kamishna Mkuu, atakuwa na jukumu la ukaguzi wa ndani wa hesabu za Mamlaka na atawasilisha kwa Kamishna Mkuu ripoti kila baada ya miezi mitatu kuhusiana na Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka wa Fedha.

Ripoti za Kamishna Mkuu.

**28.**-(1) Kamishna Mkuu atawasilisha kwa Bodi ripoti za muda kuhusiana na mapato yaliyokusanywa na idara tofauti kwa muda na kwa namna kama Bodi itakavyoamua.

(2) Kamishna Mkuu, ndani ya miezi mitatu baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, atawasilisha ripoti kwa Bodi na Bodi itawasilisha kwa Waziri kuhusiana na mwaka huo, ikijumuisha:

(a) muhtasari wa taarifa za fedha zinazoonesha ukusanyaji wa mapato chini ya wakuu na idara tofauti;

(b) taarifa ya utekelezaji wa sehemu tofauti za Mamlaka na idara za mapato;

(c) uchambuzi na sababu za kutofautiana katika mapato halisi ukilinganisha na makadirio ya bajeti; na

(d) mambo mengine kama Bodi itakavyomuelekeza Kamishna Mkuu.

Kufuta kodi isiyoweza kugombolewa.

**29.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, kuhusu kuacha madai na kufuta fedha za umma, Waziri anaweza kufuta kodi isiyogomboleka baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa Mamlaka.

(2) Mamlaka inaweza baada ya kuidhinishwa na Bodi kupendekeza kwa Waziri kwamba kodi isiyogomboleka ifutwe.

(3) Endapo mapendekezo ya kufuta kodi isiyogomboleka chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki yamefanywa, majina ya watu wanaohusika yataondolewa.

(4) Mapendekezo ya kufuta kodi isiyogomboleka yatajumuisha maelezo yafuatayo:

(a) kiasi cha kodi isiyogomboleka;

(b) tarehe tangu ambapo kodi haijalipwa;

(c) hatua za utekelezaji zilizochukuliwa;

(d) sababu za kupendekeza kufutwa; na

(e) jumla ya kiasi cha malimbikizo ya mapato.

(5) Bodi itaandaa miongozo ya ufutaji wa kodi isiyogomboleka.

Mamlaka kusamehewa kodi.

**30.** Mamlaka itasamehewa kulipa ushuru wowote, kodi au tozo kuhusiana na uingizaji, uendeshaji, mtaji, mali, nyaraka, muamala wowote, hati, makubaliano, ada au hati ya ahadi ambayo Mamlaka inahusika.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI MENGINEYO

Kinga ya kutowajibika binafsi.

**31.** Kamishna Mkuu, afisa aliyeidhinishwa au mtu mwengine yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya Mamlaka, hatowajibika binafsi katika shauri la madai kuhusiana na kufanya au kutokufanya jambo kwa nia njema katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii au sheria nyengine inayotumika.

Kuomba msaada.

**32.** Kamishna Mkuu anaweza kuomba msaada kutoka katika taasisi yoyote husika kufanya kazi maalum inayohusiana na usimamizi wa mapato ya Serikali.

Utambuzi wa walipakodi.

**33.** Mamlaka itahakikisha katika uanzishwaji, utunzaji na matumizi ya mfumo rafiki na thabiti kwa ajili ya kuwatambua walipakodi kwa madhumuni ya usimamizi mzuri wa sheria za mapato Zanzibar na itakuwa na uwezo wa kuchukua hatua stahiki katika mwelekeo huo.

Usiri.

**34.**-(1) Mjumbe wa Bodi, Kamishna Mkuu au mtu mwengine yeyote aliyeajiriwa katika kutekeleza masharti ya Sheria hii, atazingatia na kusimamia nyaraka na taarifa zote zinazohusiana na mapato, matumizi au shughuli nyengine za kifedha au hali ya mlipakodi yeyote au mtu mwengine yeyote anayehusika katika shughuli yoyote katika kufanikisha madhumuni ya Sheria hii, na maelekezo yote ya siri kuhusiana na usimamizi wa Sheria hii ambayo anaweza kuyapata au kujua wakati akitekeleza majukumu yake kama siri kwa mtu yeyote ambaye hajaidhinishwa.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itakuwa halali kwa maafisa katika Mamlaka kubadilishana au kupeana taarifa au nyaraka zinazomhusu mlipakodi yeyote kwa ajili ya utekelezaji wa kazi chini ya Sheria hii.

(3) Mamlaka inaweza kwa maslahi ya umma kuamua kuchapisha taarifa zinazohusiana na mlipakodi au kundi la walipakodi, ambayo inaona ni muhimu katika utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii.

Ukabidhiwaji wa mali na waajiriwa.

**35.**-(1) Waajiriwa wote ambao, kabla ya kuanza kutumika Sheria hii walikuwa waajiriwa wa Bodi ya Mapato Zanzibar, baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, wataendelea kuwa waajiriwa wa Mamlaka.

(2) Mali yote, isipokuwa mali yoyote ambayo Waziri ataamua mara tu kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ilikuwa chini ya Bodi ya Mapato ya Zanzibar, kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii itakuwa chini ya Mamlaka pamoja na maslahi yote, dhima, malipo, wajibu na dhamana katika mali.

Utekelezaji wa amri dhidi ya Mamlaka.

**36.** Kwa madhumuni ya Sheria hii, na bila ya kujali masharti yoyote yanayokinzana katika sheria nyengine yoyote, endapo katika shauri lolote la madai au dhidi ya Mamlaka, amri yoyote, pamoja na amri ya gharama, imetolewa na mahkama kwa ajili ya mtu yeyote dhidi ya Mamlaka au dhidi ya afisa wa Mamlaka, au endapo mahkama itatoa amri ya kukaza hukumu, kukamata au kwa utaratibu wa aina hiyo, masharti yote ya Sheria ya Mwenendo wa Madai dhidi ya Serikali yanayohusiana na utekelezaji wa amri dhidi ya Serikali yatatumika katika shauri kama kwamba shauri lilikuwa ni shauri la Serikali au dhidi ya Serikali.

Uwezo wa kurekebisha majadweli.

**37.** Waziri anaweza, kila baada ya muda, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti, kurekebisha Majadweli chini ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**38.**-(1) Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar, Nam. 7 ya 1996 inafutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitu chochote kilichofanywa au kingepaswa kufanywa chini ya masharti yoyote ya Sheria iliyofutwa, kitaendelea kuwa halali na kitachukuliwa kuwa halali na kimefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

Kanuni.

**39.** Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii."

Marekebisho yenye athari.

**40.**-(1) Sheria zote chini ya Sheria hii au sheria yoyote inayohusiana na ukusanyaji wa mapato ambayo neno "Kamishna" litaonekana litasomwa kama "Kamishna Mkuu".

(2) Sheria zote chini ya Sheria hii au sheria yoyote inayohusiana na ukusanyaji wa mapato ambayo neno "Bodi ya Mapato Zanzibar" litaonekana litasomwa kama "Mamlaka ya Mapato Zanzibar".

**JADWELI LA KWANZA**

**SHERIA ZINAZOHUSIANA NA MAPATO YA ZANZIBAR**

**[Chini ya kifungu cha 5(a)(i)]**

---

1. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998.
2. Sheria ya Ushuru wa Stamp Nam. 7 ya 2017.
3. Sheria ya Ushuru wa Hoteli, Nam. 1 ya 1995.
4. Sheria ya Tozo ya Huduma Bandarini, Nam. 2 ya 1999.
5. Sheria ya Tozo ya Petroli, Nam. 7 ya 2001.
6. Sheria ya Kodi ya Majengo, Nam. 14 ya 2008.
7. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Nam. 8 ya 2017.
8. Sheria ya Usimamizi na Taratibu za Kodi, Nam. 7 ya 2009.
9. Sheria nyengine yoyote itakayotumika au inayoweza kuanza kutumika kuhamasisha na kukusanya mapato Zanzibar.

## JADWELI LA PILI

## MWENENDO WA BODI

**(Chini ya kifungu cha 16)**

---

*Muda wa wajumbe wa Bodi.*

1. Isipokuwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

*Vikao vya Bodi.*

**2.**-(1) Bodi itakutana kila mwezi na inaweza kukutana katika vikao vya dharura muda wowote inapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti, ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao cha Bodi na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

*Akidi.*

**3.** Akidi katika vikao vyote vya Bodi itakuwa ni zaidi ya nusu ya wajumbe wake.

*Maamuzi ya Bodi.*

**4.** Maamuzi ya Bodi yatafanywa kwa maafikiano, ikiwa hakuna maafikiano, maamuzi yatafanywa kwa kura na ikitokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi.

*Taratibu za vikao.*

**5.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuandaa taratibu zake zenyewe kuhusiana na vikao na utaratibu wa kutekeleza shughuli zake ikijumuisha Kamati za Bodi.

*Mjumbe mualikwa.*

**6.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye si mjumbe wa Bodi kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya vikao vya Bodi kama mtaalamu lakini mjumbe mualikwa huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

*Kubainisha maslahi.*

7.-(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kujadiliwa na Bodi, haraka iwezekanavyo baada kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha:

(a) hatahudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya maamuzi; au

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya maamuzi.

Kusita kuwa mjumbe.

**8.** Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya kuwa na sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu za afya ya kimwili au kiakili;

(d) kusitishwa na Waziri kwa kushindwa kutimiza matarajio ya Mamlaka;

(e) ikiwa mjumbe atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyompendekeza Mjumbe huyo; au

(f) kifo.

Kukasimu kazi za Bodi

**9.**-(1) Bodi inaweza, inapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Kamati ya Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi hizo.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 14 Disemba, 2022.

..............................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi***
***Zanzibar.***